

*Kurudishia udongo shimoni.*

### 2.1 Kupanda mbegu

- Fukua vishimo viwili vyenye kina cha sentimita tano kilichochimbwa umbali wa sentimita tano kutoka kwenye mambo.
- Panda mbegu moja katika kila kishimo na ukielekeza kovu juu.

*Angalizo*

Inashauriwa wakati wa kupanda mbegu utumie korosho kutoka mavuno ya msimu husika kwa sababu hizi zinauhakika wa kuota mapema na vizuri.

### 2.2 Kupandikiza mkorosho uliobebeshwa

- Fukua shimo kwenye mambo lenye kimo cha sentimita 20 na upana wa sentimita 12 ili ipatikane nafasi kwa ajili ya kupandikiza mche.
- Weka kiriba chenye mche ndani ya shimo
- Chana kiriba kikiwa ndani ya shimo na kukiondoa bila kubomoa bonge udongo.



*Jinsi ya kupanda mche wa korosho*

- Shindilia udongo mpaka usawa wa ardhi na hakikisha sehemu iliyounganishwa haifukiwi na udongo.
- Simika mambo sentimita kumi kutoka kwenye mche.
- Baada ya miezi mitatu shikiza mche kwa kamba kwenye mambo.



*Jinsi ya kuweka mambo kwenye wa mche wa mkorosho.*



# KUPANDA MIKOROSHO MIPYA




*Kimetayarishwa na:*

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509,
MTWARA
Email : cdnaliendele@tari.go.tz


**April 2019**

# KUANZISHA SHAMBA JIPYA LA MIKOROSHO

## 1.0 Utangulizi

Upandaji wa mikorosho mipya ni kitendo cha kuanzisha shamba jipya kwa kufuata kanuni za kilimo bora cha korosho. Mashamba ya wakulima walio wengi yanatoa mavuno kidogo na hafifu. Uzaaji mdogo umetokana na matumizi ya mbegu duni za korosho na upandaji holela.

Mbegu bora za korosho na miche iliyobebeshwa hupatikana katika Vituo vya Uendelezaji Zao la Korosho ambavyo Naliendele (Mtwara), Nanyanga (Tandahimba), Nyangao (Lindi), Mangaka (Masasi), Nakayaya (Tunduru), Mkuranga (Mkuranga), Mlingano (Tanga).

Sifa za mbegu bora na mikorosho iliyobebeshwa ni kuzaa mapema, mavuno mengi na bora.



## 2.0 Kutayarisha shamba:

- Safisha eneo unalotaka kuanzisha shamba jipya
- Ng'oa visiki
- Tifua shamba kwa ngwamba, makisai au trekta.
  *Angalizo*
  Kazi hii inatakiwa ifanyike kabla ya kuanza kwa mvua za msimu.

## 2.1 Kupima shamba.

- Pima shamba kwa kuzingatia nafasi za mita 12 shimo hadi shimo na mita 12 mstari hadi mstari.



*Jinsi ya kupima shamba la korosho*

- Ikiwa kuna matarajio ya kuchanganya mazao kwa miaka mingi, tumia nafasi ya mita 12 kati mkorosho na mkorosho na mita 15 kati ya mstari na mstari.

- Kazi hii ifanyike miezi miwili hadi mitatu kabla ya mvua kuanza.



*Mfano wa shamba la korosho jipya lililochanganywa na kunde*

## 2.2 Kuandaa mashimo

- Chimba shimo lenye urefu sentimita 60, upana sentimita 60 na kimo sentimita 60.
- Chimba udongo wa juu sentimita 15 uweke kando na ule wa chini sentimita 45 uweke upande mwingine.
- Changanya udongo wa juu na samadi/mboji debe moja iliyooza vizuri au gramu 40 za NPK.
- Rudishia udongo uliochanganywa na mbolea kwanza halafu ufuate ule wa chini.
- Weka mambo katikati ya shimo.